MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA MAMLAKA YA MAPATO KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU YA MWAKA WA FEDHA 2025/26 (JANUARI HADI MACHI 2026)

Dar es Salaam, 01 Aprili, 2026

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ('TRA' au 'Mamlaka') inapenda kuutaarifu umma kuhusu utendaji kazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2025/2026 (Januari hadi Machi, 2026):

1. ULIPAJI KODI WA HIARI NA UKUSANYAJI WA KODI

Katika kipindi cha mwezi wa Machi 2026, TRA imefanikiwa kukusanya kiasi cha **shilingi trilioni 3.58** sawa na ufanisi wa **asilimia 107.6** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 3.32.** Makusanyo haya ya mwezi Machi yanapelekea TRA kuwa imekusanya kiasi cha **shilingi trilioni 9.31** sawa na ufanisi wa **asilimia 106.4** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 8.75**, katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/26 (Januari hadi Machi 2026). Makusanyo hayo ya kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/26, ni sawa na ukuaji wa **asilimia 23.6** ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi trilioni 7.53** kilichokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2024/25. **Jedwali Na. 1** linaonesha makusanyo ya kodi kwa kipindi cha robo ya tatu (Januari -Machi 2026) ya mwaka fedha 2025/26.

Jedwali Na.1: Makusanyo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwezi Januari – Machi, 2025/26 **Shilingi Trilioni**

MWEZI	MAKUSANYO 2024/25	2025/26			
		LENGO	MAKUSANYO	UFANISI	UKUAJI
Januari	2.42	2.85	3.04	106.7%	25.9%
Februari	2.27	2.57	2.69	104.4%	18.5%
Machi	2.84	3.32	3.58	107.6%	25.7%
Jumla	**7.53**	**8.75**	**9.31**	**106.4%**	**23.6%**

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania

Aidha, katika kipindi cha miezi tisa (9) ya kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, TRA imefanikiwa kukusanya jumla ya kiasi cha **shilingi trilioni 28.005 kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 26.773 ambao ni ukuaji wa asilimia 16.5**

Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, ufanisi katika usimamizi wa sheria za kodi umeimarika ambapo uwiano wa kodi kwa gharama za makusanyo ni asilimia 2.41, na uwiano wa kodi kwa pato la taifa unakadiriwa kufika asilimia 14.1 toka asilimia 13.7

2. USAJILI WA WALIPAKODI WAPYA ILI KUONGEZA WIGO WA KODI
Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, TRA ilikuwa na lengo la kusajili walipakodi wapya **685,706** ambapo mpaka kufikia tarehe 31 Machi, 2026, imefanikiwa kusajili walipakodi wapya **900,755** ambao ni ufanisi wa **asilimia 131.36.** Aidha, mpaka tarehe 31 Machi, 2026, jumla ya walipakodi waliosajiliwa ni **8,245,704.**

3. MAHUSIANO PAMOJA NA USHIRIKIANO NA WALIPAKODI
Katika kipindi cha robo ya tatu mahusiano na Viongozi wa vyama vya wafanyabiashara pamoja na wafanyabiashara wenyewe yaliimarishwa kwa kufanya mikutano na kuwasikiliza ili kutatua changamoto zao za kikodi. TRA itaendelea kuboresha mahusiano na walipakodi kwenye Shughuli zote za Kiuchumi ili kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari nchini.

TRA iliendelea kuwahudumia walipakodi siku za mapumziko **(Jumamosi & Jumapili)** kupitia ofisi zote za TRA nchini, na kushirikiana na walipakodi, kuwasikiliza na kutatua changamoto zao kila siku ya Alhamisi katika ofisi zote za TRA nchini pamoja na kupitia programu ya **MARAFIKI** na **MABALOZI WA KODI** nchini.

4. UDHIBITI WA UKWEPAJI KODI NA MAGENDO ILI KULETA USAWA
UDHIBITI WA MAGENDO: katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/26, TRA iliweza kukamata mizigo yenye thamani ya shilingi billioni 8.99, iliyowezesha kuokoa kodi ya **shilingi billioni 3.12.**

KUDHIBITI UKWEPAJI KODI: Mamlaka imeendelea kudhibiti vitendo vya ukwepaji kodi kuwa kudhibiti na kuondoa njia zinazotumika na wafanyabiashara wenye nia ya kukwepa kodi kama vile **kuficha mauzo halisi kwa kubandika stempu feki katika vinywaji changamshi, kutoa risiti zenye thamani pungufu ya kiasi halisi kilicholipwa, kutumia akaunti binafsi za benki kupokea fedha za biashara kwa lengo la kukwepa kodi.** Katika kipindi hiki, TRA imekamilisha chunguzi **393** na kuokoa kiasi cha **shilingi Bilioni 675.** Tutaendelea kuchukua hatua kali kwa mujibu wa sheria, kwa wote wanaojihusisha na vitendo vya ukwepaji kodi ili kuleta usawa katika ulipaji kodi nchini.

5. UTOAJI WA ELIMU YA KODI
Katika kipindi cha mwezi Januari – Machi 2026, TRA imefanya shughuli mbalimbali za elimu kwa walipakodi kupitia kampeni zaidi ya **1,416** zinazojumuisha elimu ya mlango kwa mlango, vipindi vya redio na televisheni, huduma kwa wateja, vilabu vya kodi mashuleni, mitandao ya kijamii, maonesho, na semina, zote zikilenga kuongeza uelewa wa masuala ya kodi kwa watanzania.

TRA itaendelea kutoa elimu ya kodi nchini kupitia kampeni mbalimbali nchini ikiwemo ufadhili wa mashindano makubwa ya michezo na kupitia timu yetu ya mpira wa miguu ya **TRA United SC** inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka - Tanzania Bara.

6. UTATUZI WA MIGOGORO YA KODI
Katika kipindi husika, TRA imeendelea na utatuzi wa migogoro ya kikodi kwa njia ya UTATUZI WA MAPINGAMIZI YA KODI (Tax objection Settlement) na UTATUZI WA MIGOGORO YA KIKODI KWA NJIA YA NJE YA MAHAKAMA (Out of Court Settlements). Katika kipindi cha mwezi Januari - Machi, 2026, TRA imetatua migogoro ya kikodi kwa utaratibu wa nje ya Mahakama (Out of Court Settlements) ya kesi **30**, yenye thamani ya kodi ya **Shilingi bilioni 800.8,** hali inayoashiria uboreshwaji wa mahusiano baina ya Mamlaka na walipakodi.

7. UENDELEZAJI WA UFANISI NA USIMAMIZI WA MAADILI KAZINI

TRA itaendelea kuweka kipaumbele kuhakikisha watumishi wote wa TRA wanazingatia weledi katika utendaji kazi ikiwemo kuwapatia mafunzo ya kuongeza weledi ambapo katika kipindi hiki watumishi **885** walipatiwa mafunzo.

TRA itaendelea kuwapongeza na kuwazawadia watumishi waliofanya vizuri na kufuata misingi ya maadili ambapo watumishi **418** katika kipindi cha robo tatu za mwaka wa fedha 2025/26 walipongezwa na kutunikiwa tuzo za ufanyakazi bora na zawadi katika Ofisi za TRA nchi nzima.

TRA itaendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wachache wanaokiuka misingi ya maadili ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, **watumishi 3 wameshushwa vyeo kwa kosa la kimaadili, watumishi 6 wameshushwa mshahara kwa kosa la kukosa uaminifu kazini, na watumishi 10 wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa makosa ya kimaadili yanayowakabili.**

8. UWEZESHAJI WA BIASHARA NCHINI

Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha, uwezeshaji wa biashara uliendelea kufanywa kupitia DAWATI LA UWEZESHAJI BIASHARA (Trade Facilitation Desk): kwa kushirikiana na TISEZA, TRA imeweza kuwasajili wawekezaji **139** na kutoa misamaha ya kodi **47** katika kipindi cha Januari – Machi 2026 ili kuchochea ongezeko la ajira, ukuaji wa shughuli za uchumi na kuongeza pato la taifa.

Aidha, katika kipindi hiki, TRA imewezesha misamaha ya kodi yenye jumla ya kiasi cha **shilingi bilioni 660.805**

Katika kuwezesha biashara, katika kipindi hiki TRA imeweza kulipa **marejesho ya kodi** yenye thamani ya kiasi cha **shilingi bilioni 893.683** ambayo yamesaidia uendeshaji wa biashara mbalimbali nchini.

9. UIMARISHAJI WA MIFUMO YA TEHAMA YA KODI ZA NDANI (IDRAS) NA YA FORODHA (TANCIS)

Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha, MFUMO JUMUISHI WA USIMAMIZI WA KODI ZA NDANI (IDRAS) ulianzishwa, TAREHE 9 FEBRUARI 2026. Mfumo huu pamoja na mambo mengine umesaidia;

Kuongezeka kwa UFANISI katika uwasilishaji wa ritani za kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa wakati, kutoka asilimia 83 kabla ya kuanza kwa mfumo mpaka kufikia asilimia 86 kwa mwezi Machi 2026.

KUSOMANA NA MIFUMO MINGINE YA TAASISI MBALIMBALI ZA SERIKALI NA BINAFSI: Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Machi, 2026, IDRAS imeunganishwa na jumla ya mifumo ya Taasisi **92,** ambapo za serikali ni **63** huku binafsi n**i 29.** Muunganiko huu umeongeza uwazi na kuboresha ubadilishanaji wa taarifa kati ya TRA na Taasisi nyingine na kupelekea kuwa na kodi zenye haki na usawa.

Aidha, katika kipindi hiki USIMAMIZI wa huduma za forodha uliimarishwa KUPITIA MATUMIZI YA MFUMO WA USIMAMIZI WA FORODHA (TANCIS) ULIOBORESHWA. Upatikanaji wa Mfumo wa huduma za Forodha umeendelea kuimarika na kupunguza muda wa uondoshwaji wa shehena za forodha ambapo uondoshaji wa shehena kutoka **siku 4-5** kwa mwaka 2024/25 mpaka **siku 2-3** kwa mwaka 2025/26 katika vituo vyote vya forodha.

Kwa bahati mbaya, tarehe 3 mwezi Machi, 2026, mfumo wa Forodha ulipata downtime, iliyosababisha kukosekana kwa huduma ya mfumo iliyoleta usumbufu kwa wateja wetu. Marejesho ya mfumo ikiwemo kutumika kwa DR- site yalifanyika ambayo yameimarisha uhakika wa upatikanaji wa huduma ya mfumo kwa wakati wote. **Tunaendelea kuimarisha uangalizi wa upatikanaji wa mifumo yetu kwa wakati.**

10. MWISHO

Katika kufanikisha hili, Menejimenti ya TRA inaendelea kutekeleza kikamilifu maagizo yote ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuhusu usimamizi wa kodi nchini na uhamasishaji wa ulipaji kodi kwa hiari na kutekeleza maelekezo yanayotokana na mapendekezo ya tume ya Mheshimiwa Rais ya maboresho ya kodi kwa mujibu wa utaratibu na maelekezo ya Serikali.

TRA inapenda KUWAHAKIKISHIA wananchi na walipakodi wote kuwa itaendelea kuboresha huduma zake na kuimarisha ushirikiano na wananchi na wadau wake wote ili kuhakikisha kuwa uwajibikaji wa hiari katika kodi unafikiwa ili kuiwezesha Serikali kutekeleza mipango ya maendeleo kwa manufaa ya Taifa zima.

Mwisho, kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wote wa TRA, **TUNAWATAKIA KHERI YA SIKUKUU YA PASAKA.**

“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”

Yusuph Juma Mwenda

Kamishna Mkuu